JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P 123,
Simu: (023) 2334013,
Nukushi: (023) 2333726
Barua pepe: rbcmtwara@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

MTWARA 23/07/2020

MKOPO UMIZA WAPUNGUA KUTOKA SHILINGI 99,765,000/= HADI SHILINGI 9,765,000/= TAKUKURU (M) MTWARA ILIPOKUTANA NA MKOPESHAJI.

Ndugu Waandishi wa Habari,

UTANGULIZI:

Nimewaita hapa kwa lengo la kuujulisha umma juu ya utendaji kazi wa TAKUKURU mkoa wa Mtwara kwa kipindi cha Aprili 2020 – Juni 2020 Utaratibu huu ni wa kawaida ambao TAKUKURU imejiwekea ili kuhakikisha kuwa umma wa Watanzania pamoja na wakazi wa mkoa wa Mtwara wanafahamu jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuzuia na kupambana na rushwa.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Katika kipindi cha Aprili 2020 – Juni 2020 TAKUKURU (M) Mtwara pamoja na taarifa zingine ilipokelewa taarifa kutoka kwa bi SHADIDA ANDREW PONERA, aliyekopa fedha kutoka kampuni ya MABOTO - Tawi la Mtwara, ambaye jumla ya deni lake la mkopo lilikuwa shilingi 9,765,000= lakini kwenye salary slip yake ilikuwa inasomeka anapaswa kukatwa shilingi

99,765,000/=. Mkopaji alifuatilia suala hili ili lirekebishwe tangu Novemba 2018 akaelezwa kwamba ni makosa ya kiuandishi asubiri kidogo atarekebishiwa lakini hadi alipofika ofisi za TAKUKURU (M) Mtwara, tarehe 21/04/2020 bado alikuwa hajarekebishiwa na deni lake lilikuwa linasomeka shilingi 93,975,000/= licha ya kutaarifu tatizo hili kwa mara ya kwanza miezi 16 iliyopita kwa uongozi wa MABOTO na kurudia mara kadhaa.

TAKUKURU ilimwita na kumhoji Meneja wa kampuni ya MABOTO tawi la Mtwara FADHILI ANGELUSI SAWALA ndipo deni hilo lilirekebishwa Mwezi Mei 2020 na 'salary slip' kwa mwezi Juni imesomeka deni la shilingi 5,390,000/=.

Natoa wito kwa Taasisi za mikopo kutenda haki na pale inapojitokeza makosa kurekebisha mara moja na sio kuwazungusha wateja wao kwa jambo ambalo linawezekana kufanyika kwa haraka.Hata hivyo tuwatake wananchi kutoa taarifa pale wanapoona hawatendewi haki katika mikopo. Bi SHADIDA ANDREW PONERA asingetoa taarifa deni hili limgeweza kugharimu mali zake zingine au hata mafao yake.

Ndugu Waandisha hi wa Habari,

Katika kipindi cha Januari 2020 hadi Machi 2020, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoa wa Mtwara iliendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya Kuzuia na Kupambana na rushwa kama yalivyotamkwa katika kifungu cha 7 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007.

Katika kipindi hicho jumla ya kesi **15** ziliendelea katika mahakama za wilaya za Mtwara, Masasi, Nanyumbu, Newala na Tandahimba. Vilevile, kesi mpya **1** ilifunguliwa, Tarehe 3/6/2020 ambayo ni **Kesi ya jinai Na.76/2020** iliyofunguliwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mtwara dhidi ya mratibu MASHA Mtwara, ALLAN PETER MKOPOKA, aliyeshitakiwa kwa makosa 29, moja la wizi,22 ya kughushi nyaraka na 6 ya kuwasilisha nyaraka zenye maelezo ya uongo. Baadhi ya makosa hayo ni pamoja na kosa la wizi wa kiasi cha shilingi 1,693,000/= Kinyume na vifungu namba 258(1) na 265 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 kama ilivyorejewa mwaka 2002, kosa la Kughushi risiti ya shilingi 450,000/= ili kuonesha kuwa asasi ya MASHA ilikodi ukumbi wa mikutano kwa kampuni ya SUDI STAR jambo alilofahamu kuwa ni uongo Kinyume na vifungu namba. 333, 335 (a),(d)(i) na 337 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 kama ilivyorejewa mwaka 2002 na kughushi risiti ya shilingi 1,008,000/= ili kuonesha kuwa asasi ya MASHA ililipa BOMA CANTEEN kwaajili ya chakula na vinywaji jambo ambalo alifahamu kuwa ni uongo Kinyume na vifungu namba. 333, 335 (a), (d)(i) na 337 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 kama ilivyorejewa mwaka 2002.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Katika kipindi cha Aprili 2020 hadi Juni 2020 jumla ya taarifa (75) za makosa ya rushwa na makosa mengine ya jinai zilipokelewa na TAKUKURU (M) Mtwara na uchunguzi wake unaendelea katika hatua mbalimbali na nyingine watuhumiwa wamefikishwa mahakamani. Mchanganuo wa Sekta au taasisi zinazolalamikiwa ni kama ifuatavyo:-

Halmashauri, malalamiko (34) katika idara zake kwa mchanganuo ufuatao:- utawala(17), afya(6), ardhi(2), elimu(2), manunuzi(2), kilimo(2), ushirika(2) na biashara(1).

Malalamiko mengine ni vyama vya Ushirika malalamiko(15), Siasa(9), Mahakama(6), Polisi(2), TRA(1), TFS(1), TANESCO(1), PSSSF(1) na binafsi (5).

Ninatoa wito kwa watumishi wa Halmashauri zote za mkoa wa Mtwara na viongozi katika vyama vya ushirika kufanya kazi kwa uadilifu na kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu kwani takwimu za taarifa za malalamiko dhidi yao ni kubwa. Aidha tumeshuhudia malalamiko ya siasa kuongezeka na naomba nisisitize wanasiasa, wasimamizi wa chaguzi na wapiga kura tuepuke rushwa kuelekea uchaguzi mkuu katika kila hatua.

Ndugu Waandishi wa Habari

Aidha katika kipindi tajwa, ili kuzuia Rushwa, tumefuatilia matumizi ya fedha za Umma katika Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa hapa mkoani Mtwara. Lengo likiwa ni kuhakikisha kwamba miradi hiyo inatekelezwa kwa kiwango kinachotakiwa na thamani ya fedha inapatikana. Jumla ya miradi ya maendeleo minane (12) yenye thamani ya jumla ya shilingi **5,128,281,675.27** ilifuatiliwa kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapa chini:-

NA	***MRADI***	***THAMANI (Tsh)***
1	*Ukarabati wa majengo TTC (kawaida) -**Mtwara***	*679,845,856.89/=*
2	*Ukarabati wa majengo TTC (ufundi) -**Mtwara***	*641,645,904/=*

3	*Ukarabati wa majengo ya shule ya wasichana Mtwara -* ***Mtwara***	*776,605,047/=*
4	*Ukarabati wa Hosipitali ya wilaya Nanyumbu (jingo la uzazi) -****Nanyumbu***	*400,000,000/=*
5	*Mradi wa maji Nandete -* ***Nanyumbu***	*338,922,298.66/=*
6	*Mradi wa Barabara Tandahimba-Mivanga (8km)-* ***Tandahimba****.*	*177,495,460/=*
7	*Mradi wa Barabara Tandahimba- Nachungumla(9.5km)-* ***Tandahimba.***	*112,011,726/=*
8	*Mradi wa maji Jangwani-Makeka-* ***Tandahimba.***	*1,253,673,300/=*
9	*Mradi wa ukamilishaji wa boma madarasa mawili na ofisi shule ya sekondari Makukwe-****Newala***	*52,458,550/=*
10	*Mradi wa ukamilishaji wa boma madarasa mawili na ofisi shule ya sekondari Mpotola-* ***Newala***	*52,458,550/=*
11	*Mradi wa maji Mitema –Mtongwele -****Newala***	*621,305,960/=*
12	*Ufuatiliaji fedha za ruzuku shule za msingi -****Tandahimba***	*21,859,022.72/=*

Katika miradi tajwa iliyofuatiliwa, mradi wa ukarabati wa hosipitali ya wilaya ya Nanyumbu (jengo la Uzazi) umeonekana kuwa na tatizo la manunuzi hewa ya vifaa vya thamani ya Tsh. 54,000,000/= na uchunguzi umeanzishwa.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Katika kuhakikisha kuwa TAKUKURU inashirikisha umma katika mapambano dhidi ya Rushwa, shughuli za kuelimisha Umma katika kipindi tajwa zilifanyika kwa kuendesha Semina 18, mikutano ya hadhara 53, Kufungua na kuimarisha Klabu 15 za wapinga rushwa katika shule za Sekondari na vyuo, Uandishi wa makala 10, Kuelimisha kupitia vipindi vya redio 02 na kutoa taarifa 3 kwa umma kupitia vyombo vya habari.

Aidha jumla ya machapisho 472 yenye elimu dhidi ya rushwa yaligawiwa kwa wananchi

Ndugu Waandishi wa Habari,

Katika kipindi cha kuanzia , Julai 2020 hadi septemba 2020, mikakati ya TAKUKURU Mtwara katika kuzuia na kupambana na rushwa ni pamoja na yafuatayo;

- Kuendelea kutoa elimu kwa umma kwa lengo la kuwafanya wananchi kuchukua hatua na kushiriki mapambano dhidi ya Rushwa na kuacha kuwa walalamikaji tu.
- Kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa kuelekea uchaguzi mkuu na katika tasnia ya korosho kwa kuhakikisha kila mkulima anapata stahiki yake.
- Kuendelea kufuatilia matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo ya wananchi katika sekta za kimkakati za maji, afya, elimu na ujenzi (barabara).
- Kuendelea kufanya chambuzi za mifumo ili kubaini sababu zinazosababisha kuwepo kwa Rushwa na kutoa ushauri wa namna ya kurekebisha au kuboresha na hatimaye kutoa huduma bora.

SHUKRANI:

TAKUKURU (M) wa Mtwara inapenda kuwashukuru wananchi na wadau wote kwa ushirikiano wanaotupatia katika shughhuli zetu na tunaomba tuendelee na moyo huu wa kizalendo.

Pia napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Ndugu waandishi wa habari kwa ushirikiano wenu na pia nizidi kuwaomba kutuunga mkono katika kutekeleza majukumu yetu kwa kutupatia fursa katika vyombo vyenu ili kuwaelimisha wananchi kuhusu athari na madhara ya rushwa na namna salama na rahisi ya kukabiliana nayo.

"**Kataa Rushwa, Jenga Tanzania"**

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

ENOCK P. NGAILO
KAMANDA WA TAKUKURU (M) MTWARA